بسم الله الرّحمن الرّحيم

Kwa jina la Allah,
Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu

Visa vya Kweli 1

Hifadhi Iliyokataliwa

Mtungaji
Ustadh Shahid Murtadha Mutahhari

Mtarjumi
S. Muhammad Ridha Shushtary

Mchapishaji
ISLAMIC THOUGHT FOUNDATION
No.5, Takhti Sq., Shahid Beheshti Ave.
P.O. Box 14155-3899
Tehran
Islamic Republic of Iran
Tel: 844092-5, Fax: 898295, Telex: 216502 ISTF

مصونیتی که لغو شد

از کتاب داستان راستان

نوشته

استاد شهید مرتضی مطهّری

ترجمه به سواحلی

سیّد محمّدرضا شوشتری

SAW: Sallallaahu ‘Alayhi Wa-aalih, m.y. baraka na rehema za Allah ziwe kwake na kwa Aali zake.
AS: ‘Alayhi/‘Alayha/‘Alayhuma’s Salaam, m.y. amani iwe juu yake/yao.

Jina la kitabu: *Hifadhi Iliyokataliwa*
Mtungaji: *Ustadh Shahid Murtadha Mutahhari*
Mtarjumi: *S. Muhammad Ridha Shushtary*
Mchoraji: *Sadiq Sanduqi*
Mpangaji: *Muhammad Abu Shahab*
Lugha ya asili ya kitabu: *Kifarsi (Kiajemi)*
Mpangiliajichapa: *Idara ya Usanii ya Taasisi ya Fikra za Kislamu*
Mchapishaji: *Taasisi ya Fikra za Kiislamu*
Idadi ya nakala: *5,000*
Chapa: *Ya kwanza*
Tarehe ya uchapaji: *1415 Hijria (1995)*

Waislamu waliohama Makka na kwenda Uhabeshi kutokana na mateso na maonevu waliyokuwa wakifanyiwa na Maqureshi, kila siku walikuwa wakitazamia kusikia habari mpya kutoka Makka na kwa Wamakka. Ingawa

idadi yao na ya wenzao walio wafuasi wa Tawhidi (Umoja wa Mungu) na uadilifu ilikuwa ndogo sana ikilinganishwa na idadi kubwa ya wapinzani wao – yaani wafuasi wa ushirikina na wanaopendelea uendeleaji wa mfumo huo wa jamii – lakini walikuwa na matumaini kwamba idadi ya wawaungao mkono itazidi kila siku, na idadi ya wapinzani itapungua. Hawa-

kuvunjika moyo hata kidogo juu ya upinzani wa Maqureshi, bali walikuwa na matumaini kwamba karibuni Maqureshi wote watatoka katika ujinga na watafuata njia ya uongofu na ya manufaa kwa ajili yao, na watawafuata wao katika kuacha itikadi za kuabudu masanamu, na badala yake watasilimu.

Kwa bahati, habari ikavuma katika mahali walipokuwa wakiishi huko Uhabeshi kwamba Maqureshi wote wamebadilisha itikadi zao na wamechagua Uislamu kuwa ni dini yao. Ingawa habari hiyo haikuthibitishwa rasmi lakini kutokana na imani, itikadi na matumaini makubwa



waliyokuwa nayo juu ya kusambaa na kushinda dini ya Kiislamu, kikatoka kikundi kimoja cha Waislamu hao kurejea Makka bila hata ya kungoja kuhakikishwa habari hiyo. Mmojawapo kati ya wahijiri hao alikuwa sahaba mashuhuri aitwaye Uthman bin Madh'un ambaye alikuwa



akimpenda Mtume Mtukufu kupita kiasi, na alikuwa akiheshimiwa na Waislamu wote. Uthman bin Madh'un alipokaribia mji wa Makka, aling'amua kwamba habari hiyo ilikuwa ya uwongo, na kinyume chake, Maqureshi walizidi kuwatesa Waislamu. Hivyo, hakuwa na njia ya kwenda mbele wala kurejea, kwa sababu Uhabeshi haikuwa karibu wala haikuwa kazi rahisi kuweza kurejea huko. Kwa upande mwingine, kuingia Makka kulikuwa ni sawa na kukabiliana



na hali hiyohiyo. Mwishowe, ikamjia fikra moja, nayo ni kutumia mila na desturi ya Waarabu ya kuomba hifadhi ya Mqureshi mmoja mwenye satua na nguvu katika jamii.

Kwa mujibu wa mila ya Kiarabu, ikiwa mtu ataomba hifadhi au kinga kutoka kwa mtu mwingine ili amlinde na amtetee, basi mtu huyo atawajibika amhifadhi hata kama kwa kufidia roho yake. Ilikuwa ni aibu kwa Mwarabu,

mtu amwombe hifadhi kisha amkatalie – hata kama ni adui yake -- au baada ya kumpa hifadhi, asimlinde. Basi Uthman akaingia mjini Makka usiku wa manane, na moja kwa moja alikwenda nyumbani kwa Walid bin Mughira Makhzumi, ambaye alikuwa ni miongoni mwa watu mashuhuri, mabepari na wenye satua katika kabila la Kiqureshi, na akamtaka ampe hifadhi. Walid akamkubalia.

Siku ya pili, Walid bin Mughira akamchukua Uthman bin Madh'un katika Masjidul Haram wakati wakuu wa Kiqureshi walipokuwa wamekusanyika hapo; na akatangaza rasmi kwamba tangu sasa Uthman yupo chini ya hifadhi yake,

na yeyote atakayemsumbua, atakuwa kama amemsumbua yeye binafsi. Kwa kuwa Maqureshi waliiheshimu hifadhi ya Walid bin Mughira, hivyo, hawakumsumbua tena Uthman. Tangu saa hiyo alipopata hifadhi, Uthman alikuwa akitembea kwa uhuru, na akishiriki katika mabaraza ya Maqureshi kama mmoja wao.

Lakini kwa wakati huohuo, Maqureshi hawakusita kuwaonea na kuwatesa Waislamu wengine. Hali hii ya kuona wenzake wana-sumbuliwa ilimkera sana Uthman. Siku moja akafikiri: "Hii si murua kwangu mimi nipate raha katika hifadhi ya mshirikina mmoja, na ndugu zangu wenye fikra na itikadi kama zangu waonewe na wateswe." Kwa sababu hii akaenda kwa Walid bin Mughira na kumwambia:

"Mimi nakushukuru sana kwa kunipa hifadhi yako na kunihami, lakini tangu leo nataka kujitoa katika hifadhi yako na kujiunga na wenzangu. Wacha lolote linalowafika wao linifike mimi pia."

"Mwanangu, labda hukuridhika au hifadhi yangu haikukupa usalama."



"Si kwa sababu hiyo, ila mimi nataka tangu sasa nisiwe chini ya hifadhi na himaya ya mtu yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu tu."

"Ilivyokuwa umeamua hivyo, basi kama vile siku ya kwanza mimi nilikuchukua Masjidul Haram na nikatangaza rasmi mbele ya Maqureshi kukupa himaya yangu, hivyo, twende tena Masjidul Haram nitangaze rasmi mbele ya Maqureshi kutoka kwako katika hifadhi yangu."

"Vizuri sana, sina pingamizi."



Walid na Uthman wakaingia katika Masjidul Haram. Wazee wa Kiqureshi walipokusanyika, Walid akasema: "Nyote mjue kwamba Uthman amekuja hapa kutangaza kutoka kwake katika hifadhi yangu."

Uthman akasema: "Amesema kweli. Mimi nimekuja hapa kwa ajili hilo, na ninaongeza kusema kwamba katika muda wote niliokuwa katika himaya ya Walid, amenitendea vizuri, na kwa sababu hii mimi nimeridhika. Sababu ya kutoka kwangu katika hifadhi yake ni hii tu kwamba sipendi kuwa chini ya hifadhi ya mtu yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu tu."

Kwa hivyo, muda wa hifadhi ya Uthman ukamalizika, na kinga aliyopata mpaka wakati ule ikaondoka. Lakini Uthman aliendelea bila ya wasiwasi kuhudhuria katika baraza la Maqureshi kama zamani.

Kwa bahati, katika siku zile, Labiid bin Rabii'ah, aliyekuwa mshairi mashuhuri katika Bara Arabu alikuja Makka. Lengo lake lilikuwa ni kusoma katika baraza la Maqureshi shairi lake mpya ambalo linasifikana kuwa ni mojawapo kati ya mashairi bora kabisa ya zama za Ujahilia wa Kiarabu. Shairi la Labiid linaanza kwa ubeti huu:

Alaa kullu shay'in
maa khala 'l-Laahu baatilu
Kila kitu ni batili
ila Mungu wa azali.

Kuhusu ubeti huu, Mtume Mtukufu amesema: "Huu ni ubeti wenye ukweli kabisa ambao haujapata kutungwa na Waarabu."

Labiid akaingia katika baraza la Maqureshi ili kusoma shairi lake. Hadhirina walikaa kimya kusikiliza shairi hilo lililotia fora. Naye Labiid akaanza kusoma kwa maringo na ufakhari:

Alaa kullu shay'in
maa khala 'l-Laahu baatilu
Kila kitu ni batili
ila Mungu wa azali.

Kabla hajaanza kusoma ubeti wa pili, Uthman bin Madh'un ambaye alikuwa amekaa pembeni, akamshangilia kwa kusema: "Heko! Ukweli ndio huohuo. Kila kitu ni bure isipokuwa Mwenyezi Mungu."

Labiid akasoma ubeti wa pili:

Wa kullu na'iimin
laa muhaalata zaailu
Waama kila neema
haitabaki daima.

Uthman akapiga ukelele: "Huu ni uwongo! Si kila neema itapotea. Ni kweli kwa neema za duniani tu, lakini neema za Akhera zitabaki milele."

Watu wote walishangaa na kumtazama Uthman bin Madh'un, mtu aliye jasiri. Hakuna mtu aliyetaraji kwamba mtu lofa kama Uthman ambaye mpaka masaa machache yaliyopita alikuwa chini ya hifadhi ya mtu mwingine, na ambaye hakuwa na usalama wa maisha yake,

bali wenzake wote walikuwa wakiteswa, angethubutu kudhihirisha itikadi yake na kupinga shairi la mshairi mwenye hadhi kama Labiid bin Rabii'ah ambaye alikuja katika baraza la wazee na watukufu wa Kiqureshi kusoma shairi lake la kuvutia.

Watu wakamwomba Labiid asome tena shairi lake. Labiid alipomaliza kusoma ubeti wa kwanza tu, Uthman akasema: "Sawa! Kweli!"



Lakini Labiid aliposoma ubeti wa pili:

Wa kullu na'iimin
laa muhaalata zaailu
Waama kila neema
haitabaki daima.

Uthman akasema: "Uwongo! Si hivyo! Neema za Akhera hazitaangamia."

Mara hii Labiid akahamaki kuliko wote, na kwa sauti kubwa akasema: "Enyi Maqureshi! Naapa kwa Mwenyezi Mungu, baraza lenu halikuwa hivi zamani. Hawakuwepo miongoni mwenu watu wajuvi na wasio na adabu kama hawa. Imekuwaje sasa watu kama hawa wanaonekana miongoni mwenu?"

Mmoja kati ya watu wa barazani kwa kutaka kumtuliza Labiid na kumtaka aendelee kusoma shairi lake, alimwambia: "Usichukulie maneno ya mtu huyu. Huyu ni mpumbavu, tena yeye hayuko peke yake. Kimetokeza kikundi kimoja cha wapumbavu hapa mjini ambao wana fikra moja na huyu. Hao wameacha dini yetu na wanafuata dini nyingine."

Uthman akamjibu mtu huyo maneno makali. Naye hakuweza kustahamili, akaondoka mahali pake na akambandika kibao kimoja kwenye uso wa Uthman na jicho lake likawa jeusi. Mmoja wa hadhirina akasema:

"Uthman! Wewe hukuithamini hifadhi nzuri ya mtu. Ungebakia katika hifadhi ya Walid bin Mughira, jicho lako lisingekuwa jeusi."

Uthman akajibu:

"Hifadhi ya Mwenyezi Mungu ni salama zaidi na yenye heshima zaidi kuliko hifadhi ya mtu mwingine. Ama kuhusu jicho langu, jua kwamba jicho jingine pia lina matumaini ya kupata heshima kama lilivyopata jicho hili."

Walid bin Mughira mwenyewe akaja mbele na kumwambia:

"Uthman! "Mimi nipo tayari kukuweka tena chini ya hifadhi yangu."

"Lakini mimi nimeamua nisichukue hifadhi ya mtu yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu tu."

* * *



MASIHI NA DERAYA YA ALI

Katika zama ya ukhalifa wa Imam Ali AS, deraya (nguo ya vita inayotengenezwa kwa chuma) ya Imam ilipotea katika mji wa Kufa (Iraq). Baada ya muda deraya hiyo ilionekana kwa Masihi (Mkristo) mmoja. Ali alimpeleka kwa kadhi na kumshtaki kwa kusema kwamba: "Hii deraya ni mali yangu. Sikuiuza wala sikumgawia mtu yeyote. Na sasa nimeiona kwa mtu huyu." Kadhi akamwuliza Mkristo: "Khalifa ametoa madai yake, je, wewe unasema nini?"

Masihi akajibu: "Deraya hii ni mali yangu mwenyewe, lakini kwa wakati huohuo mimi sipingi cheo cha ukhalifa, kwani huenda khalifa amekosea."

Kadhi akamwangalia Ali na akamwambia: "Wewe unadai na huyu anakataa, hivyo, lete shahidi kuthibitisha dai lako."

Ali akacheka na kusema: "Kadhi anasema kweli. Lazima mimi nilete shahidi lakini sina."

Kwa sababu ya mshtaki kukosa shahidi, kadhi akatoa hukumu kwamba deraya ibaki kwa Masihi.

Lakini Mkristo huyo ambaye alikuwa akijua vizuri kwamba deraya ilikuwa ni mali ya nani, baada ya kwenda hatua chache akili yake ilimzunguka, akarejea na kusema: "Namna hukumu inavyoendeshwa ni tofauti na hukumu za kikawaida. Hii ni kama hukumu ya manabii." Na akakiri kwamba deraya hiyo ilikuwa ya Ali.

Haukupita muda Mkristo huyo akawa Mwislamu, na kwa shauku na imani akajiunga na jeshi la Ali katika vita vya Nahrawan.

* * *